



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb.Na. 126/290/01/21

07.01.2025

Yah:- TANGAZO LA MAFUNZO KWA WABORESHAJI WA DAFTARI LA
KUDUMU LA WAPIGA KURA 2025

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Afisa Mwandikishaji wa Jimbo la Lupembe kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 12(10)(c) cha kanuni za uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura za mwaka 2024, anapenda kuwaarifu kuwa tarehe 09-10/01/2025 wale wote waliofanya usaili na kufaulu kwa nafasi za kazi ya Wandishi Wasaidizi na Waendeshaji wa Vifaa vya Bayometriki (BVR) kuhudhuri mafunzo yatakayotolewa na Wakufunzi Kitarafa.

Tarafa ya Lupembe mafunzo yatatolewa **09-10/01/2025 katika ukumbi wa Matembwe Katani** na Tarafa ya Makambako mafunzo yatatolewa Ukumbi wa **Shule ya Sekondari Mtwango tarehe 09-10/01/2025** kuanzia saa 2.00 asubuhi, Washiriki wazingatie muda.

CASSIAN L. NKUNGA
AFISA MWANDIKISHAJI
JIMBO LA LUPEMBE